WIZARA YA NISHATI

# NewsBulletin

HABARI ZA NISHATI

Toleo Namba 67 | Jun 1 - 30 2025



# RAIS SAMIA ATAJA MAFANIKIO SEKTA YA NISHATI 2020-2025

WIZARA YA NISHATI

+255-26-2320148 AU +255-26-232018

WIZARA YA NISHATI

# BODI YA UHARIRI

## MWENYEKITI
Mhandisi Felchesmi Mramba

## MAKAMU MWENYEKITI
Dkt. James Mataragio
Dkt. Khatibu Kazungu

## MHARIRI
Neema Chalila Mbuja
Teresia Mhagama

## WAANDISHI
Timotheo Mathayo
Zuwena Msuya
Immaculate Makilika
Felista Charles

## WAPIGA PICHA
Henry Kilasila
Godfrey Mwemezi
Ruben Richard
Amanzi Kimonjo
Mustafa Shahame

## MSANIFU KURASA
Brian Mbaga

© NISHATI 2025

# RAIS SAMIA ATAJA MAFANIKIO SEKTA YA NISHATI 2020-2025

- Ni wakati akihitimisha shughuli za Bunge jijini Dodoma
- JNHPP, Umeme Vijijini, Umeme wa Gridi Kigoma na Katavi; Ni baadhi ya Vielelezo vya mafanikio
- Ataja miradi mikubwa ya usafirishaji umeme iliyokamilika
- Ataka TANESCO kuanza kuiangalia Nyukilia kama moja ya vyanzo vya kuzalisha umeme nchini.




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameeleza kuwa Sekta ya Nishati imekuwa na mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka mitano.

Ameyasema hayo wakati akihitimisha shughuli za Bunge Jijini Dodoma tarehe 28 Juni 2025.

"Mheshimiwa Spika kutokana na umuhimu wa Sekta ya Nishati kwa maendeleo ya nchi, Serikali imeimarisha upatikanaji wa nishati nchini ikiwemo kukamilisha mradi wa bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere (JNHPP)". Amesema Mhe. Samia

Ameongeza kuwa, mbali ya kukamirisha mradi wa Julius Nyerere pia Serikali imekamilisha upelekaji wa umeme katika Vijiji vyote 12,318 nchini.

Ameongeza kuwa, msukumo uliofanywa na Serikali katika sekta ya nishati umewezesha uzalishaji wa umeme kuongezeka hadi kufikia megawati 4031.71 kutoka megawati 1,601.84 mwaka 2020.



"Hali hii imechangiwa na miradi mbalimbali ya uzalishaji umeme ukiwemo mradi wa kielelezo wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere wenye megawati 2115, vilevile mradi wa Kinyerezi I Extension wa megawati 185 na mradi wa Rusumo ambao tumeutekeleza kwa ushirikiano wa Nchi tatu za Tanzania, Burundi na Rwanda kwa mgawanyo wa megawati 26.67 kwa kila Nchi". Amesema Rais Samia

Katika miradi ya usafirishaji umeme amesema Serikali imekamilisha miradi ya usafirishaji umeme ya kutoka Singida hadi Arusha, Geita hadi Nyakanazi, na Julius Nyerere hadi Chalinze.

Miradi mingine ni Nyakanazi hadi Kigoma, Tabora hadi Urambo, Rusumo hadi Nyakanazi na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kwenye njia ya Reli.

Amesema mafanikio hayo yameongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika katika maeneo mbalimbali nchini.

Aidha ameeleza kuwa, Serikali imefanikiwa kuiunganisha mikoa ya Kigoma na Katavi na gridi ya Taifa.

Kuhusu umeme Vijijini, Rais Samia amesema Tanzania imefikia hatua kubwa na ya kihistoria kwa kuunganisha Vijiji vyote 12,318 vya Tanzania Bara na huduma ya umeme.

Amesisitiza kuwa, kwa sasa Serikali inapeleka umeme kwenye Vitongoji ambapo vitongoji 33,657 tayari vimeshafikishiwa umeme kati ya Vitongoji 64,359 sawa na asilimia 52.3.

Kuhusu nishati mbadala, amesema Serikali inampango wa kuzalisha nishati mbadala kwa kutumia vyanzo jadidifu ambapo amemuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO kuanza kufikiria kuanza kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya Nyukilia.

Katika hatua nyingine, Rais Samia amesema Serikali inapanga kuweka ushindani katika Sekta ya nishati kwa kuialika sekta binafsi kushiriki kuongeza upatikanaji wa umeme.

# MEATU MTAENDELEA KUPATA MIRADI MIKUBWA YA MAENDELEO IKIWEMO NISHATI - DKT.SAMIA

- Asema baada ya Vijiji vyote Meatu kupata umeme kasi inaelekea vitongojini
- Ataka umeme utumike kuongeza thamani ya mazao, kilimo na ufugaji.




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassani amesema Serikali imeendelea kupeleka maendeleo katika Wilaya ya Meatu ikiwemo ukamilishaji wa usambazaji umeme katika Vijiji vyote 109 vya Wilaya hiyo.

Dkt. Samia ameyasema hayo Juni 17, 2025 Wilayani Meatu Mkoa wa Simiyu akiwa kwenye ziara ya kikazi.

"Kama tulivyoahidi, hatujaishia hapo, kazi ya usambazaji umeme sasa inaendelea kwenye vitongoji lakini pamoja na jitihada hizi zote ninafahamu kuna changamoto ya umeme kutokuwa na nguvu ambayo inatatuliwa." Amesema Dkt. Samia

Ameeleza kuwa, Wizara ya Nishati inatatua changamoto hiyo ya umeme kutokuwa na nguvu kwa kujenga njia ya kusafirisha umeme kutoka Shinyanga hadi Simiyu na ujenzi wa kituo cha kupokea na kupoza umeme.

Amesema kukamilika kwa miradi hiyo kutapelekea uwepo wa umeme wenye nguvu na wa kutosha kwa ajili ya shughuli mbalimbali za uzalishaji ikiwemo Viwanda.

Amesisitiza kuwa, lengo la Serikali ni kuona wananchi wanatumia nishati ya umeme kwa shughuli mbalimbali ikiwemo kuongeza thamani ya mazao, kilimo na ufugaji.

# TAASISI 762 ZATUMIA NISHATI SAFI YA KUPIKIA NCHINI - DKT.MPANGO

- Taasisi chini ya Wizara ya Nishati zapewa tuzo kutambua mchango wao katika Nishati Safi ya Kupikia na Utunzaji mazingira kupitia Gesi, Umeme



Makamu Wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango ameeleza kuwa jumla ya taasisi 762 nchini zinatumia nishati safi ya kupikia ikiwa ni jitihada za kuepuka athari za kimazingira, kiafya, kijamii na kiuchumi.

Amesema hayo tarehe 5 Juni 2025 katika kilele cha Siku ya Mazingira Duniani ambayo kitaifa imeadhimishwa jijini Dodoma katika kituo cha Mikutano cha Jakaya Kikwete.

"Taasisi nyingi za Serikali na Binafsi zimeanza kutekeleza katazo la matumizi ya nishati isiyo safi na kuanza kutumia nishati safi ya kupikia ambapo hadi Machi 2025 jumla ya Taasisi 762 zilikuwa zimeanza kutumia nishati safi ya kupikia." Amesema Dkt. Mpango







Ameongeza kuwa, kati ya taasisi hizo, taaisisi za Umma ni 495 na taasisi binafsi ni 267.i

Makamu wa Rais amempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa kinara wa kuendeleza na kusukuma matumizi ya nishati safi ya kupikia Tanzania, Afrika na Duniani kwa ujumla.

Sambamba na hilo Dkt. Mpango amezipongeza taasisi zote zilizotekeleza katazo hilo la kutotumia nishati isiyo safi na kutoa rai kwa taasisi ambazo hazijatekeleza agizo hilo ziendelee kuwekeza katika matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Katika hafla hiyo ya Siku ya Mazingira dunian, Dkt. Mpango ametoa Tuzo kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati ikiwa upande wa REA tuzo imepokelewa na Kaimu Mkurugenzi wa Usimamizi wa Rasilimali Watu na Utawala wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Bw. Renatus Msangira tuzo ya kutambua mchango wa REA katika kutunza mazingira kupitia utekelezaji wa miradi ya nishati safi ya kupikia.

Miradi hiyo ambayo ni utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia ni pamoja na usambazaji wa mitungi ya gesi pamoja na majiko banifu kwa bei ya ruzuku kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa nishati safi ya kupikia vijijini .

Aidha, TANESCO tuzo hiyo imepokelewa na Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Bw. Lazaro Twange,ikiwa ni kutambua mchango wa TANESCO katika kuhifadhi mazingira kupitia utekelezaji wa Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), ambao umeendelea kuzingatia misingi ya utunzaji wa mazingira sambamba na kuchangia kupunguza gesi joto.

Huku, CPA Mussa M. Makame - Mkurugenzi Mtendaji TPDC, amepokea TUZO ya kutambua mchango wa TPDC katika kuhifadhi na kutunza mazingiza kupitia matumizi ya gesi asilia iliyoshindiliwa (CNG).



# DKT. BITEKO AZINDUA MKAKATI WA TAIFA WA MAWASILIANO WA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

- Aagiza usiishie kwenye makabati; ukatekelezwa katika ngazi zote za Serikali/Wadau
- Atoa wito kwa vyombo vya Habari kuwa mstari wa mbele uhamasishaji wa Nishati Safi ya Kupikia
- Asema Ajenda ya Rais Samia imeonesha mafanikio; Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia yaongezeka kutoka 6% mpaka 16%



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amezindua Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano wa Nishati Safi ya Kupikia, pamoja na Kampeni ya Kitaifa ya Uhamasishaji na Uelimishaji kuhusu Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia lengo likiwa ni kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia na hivyo kuwezesha asilimia 80 ya Watanzania kuhamia katika matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia ifikapo 2034.

Akizindua Mkakati huo wa Mawasiliano jijini Dodoma, tarehe 2 Juni 2025, Dkt. Biteko ameagiza kuwa mkakati huo usiishie kukaa kwenye makabati bali utekelezwe katika ngazi zote za Serikali hadi ngazi ya mtaa bila kusahau Sekta binafsi, wadau wa maendeleo pamoja na vyombo vya Habari kuwa mstari wa mbele katika kuutekeleza.

Katika uzinduzi huo, Dkt. Biteko amempongeza Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa kinara namba moja wa matumizi ya Nishati safi ya kupikia ndani na nje ya nchi ambapo kutoka azindue Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati safi ya kupikia (2024-2034) mnamo tarehe 08 Mei, 2024 matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia nchini yameongezeka kutoka asilimia 6 hadi 16.

" Katika kuthibitisha jinsi anavyolipa umuhimu suala hili la Nishati Safi ya Kupikia, Mheshimiwa Rais pia ameunda Kitengo cha Nishati Safi ya Kupikia ambacho kina jukumu maalumu la kusimamia ajenda ya nishati safi ya kupikia na kwa kupitia kitengo hiki Serikali itaendelea na shughuli mbalimbali ikiwemo kubuni na kusimamia miradi, pia kusimamia kampeni zote za Kitaifa za uelimishaji na uhamasishaji wa nishati safi ya kupikia." Amesema Dkt. Biteko

Dkt. Biteko ameeleza kuwa, matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia yanaendelea kuathiri afya na maisha ya watumiaji wengi hasa kina mama na watoto chini ya umri wa miaka mitano ambapo taarifa zinaonesha kuwa, watu bilioni 2.1 sawa na asilimia 24.7 ya Watu wote Duniani hawana nishati safi ya kupikia ambapo kati yao watu Milioni 990 sawa asilimia 47.1 ya wanaotumia nishati isiyo salama wanatoka barani Afrika.

Ameeleza kuwa, Afrika inalazimika kufunga mkanda katika safari ndefu ya kuelekea kwenye matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia ambapo kwa upande wa Tanzania amesema kuwa kila




Taasisi inapaswa kutambua na kutekeleza jukumu lake kikamilifu.

Dkt. Biteko amewasisitiza Wadau wote wanaohusika na Nishati Safi ya Kupikia kuhakikisha kuwa wanandaa na kutekeleza Kampeni zinazolenga makundi maalum katika jamii, kukuza uelewa wa umma kuhusu njia za ufadhili na gharama nafuu, kuhakikisha ujumbe thabiti wenye kueleweka unafika kwa wadau wote na kuendeleza na kuimarisha njia za mawasiliano za kuaminika.

Katika hatua nyingine, Dkt. Biteko ameiagiza Wizara ya Nishati kupitia Kitengo cha Tathmini na Ufuatiliaji kufanya tathmini katika kila robo mwaka ili kuweza kujipima juu ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule amempongeza Rais, Dkt. Samia kwa kuendelea kuonesha kuwa nishati safi ya kupikia si suala la maneno bali ni vitendo na ndio maana anatambulika duniani kama kinara wa nishati safi ya kupikia.

Amesema kuwa suala la Nishati Safi ya Kupikia ni kipaumbele cha Mkoa wa Dodoma ambapo juhudi mbalimbali zinachukuliwa kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia akitoa mfano kuwa kwa Mkoa wa Dodoma kwa sasa tayari magereza 9 yanatumia nishati safi ya kupikia, shule za VETA 3 na shule 9 za bweni huku kazi ya uhamasishaji ikiendelea.

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga amesema katika kipindi cha miaka minne sekta ya Nishati imekuwa mashuhuri kwa masuala mbalimbali kubwa likiwa ni nishati safi ya kupikia na kueleza kuwa nguvu ya ushawishi ya Rais, Dkt.Samia imefanya ajenda ya nishati safi ya kupikia kukubalika








ndani na nje ya nchi na hivyo kutoa hakikisho la usalama wa afya za wananchi na mazingira pia.

Ameongeza kuwa Mkakati wa Mawasiliano wa Nishati Safi ya Kupikia uliozinduliwa utaongeza kasi za programu za nishati safi ya kupikia na kuleta mapinduzi ya kuhama kutoka matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia kwenda kwenye nishati safi ya kupikia.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba amesema kuzinduliwa kwa Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano wa Nishati Safi ya Kupikia ni hatua muhimu katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia.

Ameeleza kuwa Mkakati huo umeandaliwa na Wizara ya Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Mitaji la Umoja wa Mataifa (UNCDF) chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU) ambapo Mkakati huo unaongozwa na kaulimbiu ya kitaifa isemayo "Nishati Safi ya Kupikia, Okoa Maisha na Mazingira",

Amesema lengo kuu la mkakati ni kuongeza uelewa wa wananchi na taasisi kuhusu umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia na malengo mengine mahususi ni kuandaa na kutekeleza kampeni maalum za uhamasishaji wa matumizi ya nishati safi ya kupikia, kuhakikisha ujumbe wenye lengo la pamoja unafika kwa wadau wote pamoja na kuendeleza na kuimarisha njia za mawasiliano.

Naye, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. David Mathayo amempongeza Rais, Dkt. Samia kwa kuanzisha gurudumu la Nishati Safi ya Kupikia, pia amempongeza Dkt. Biteko kwa jinsi anavyoongoza Wizara na kutoa ushirikiano kwa kamati hiyo.

Aidha, Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, Rodney Thadeus amesema kuwa Wizara hiyo itahakikisha mkakati wa mawasiliano uliozinduliwa unatekelezwa kwa mafanikio kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati pamoja na wadau wengine vikiwemo vyombo vya Habari.

Vilevile, Mshauri wa Rais ( Nishati Safi ya Kupikia na Maendeleo ya Jamii) Angellah Kairuki amepongeza juhudi za serikali katika kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia hukukielelezo mojawapo kikiwa ni uzinduzi wa mkakati wa mawasiliano ambao ni muhimu katika kufikisha ujumbe kwa umma kuhusu umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Naye, Lamine Diallo, Mkuu wa Kitengo cha Rasilimali kutoka Umoja wa Ulaya ( EU), ameipongeza Wizara ya Nishati kwa tukio hilo muhimu la kuzindua Mkakati wa Mawasiliano wa Nishati Safi ya Kupikia na kusema kuwa inaonesha kwa vitendo juhudi za Serikali katika kuboresha maisha ya wananchi kupitia Nishati Safi ya Kupikia.

# UTENDAJI KAZI WA WIZARA YA NISHATI NA TAASISI ZAKE WAIMARIKA KWA ZAIDI YA ASILIMIA 95

- Dkt. Biteko apongeza; akumbusha Watendaji umuhimu wa tathmini katika kuboresha utendaji kazi
- Ataka TANESCO kuendelea kuboresha miundombinu ya umeme; kubuni vyanzo vipya
- Aziagiza Taasisi chini ya Wizara kuungana kuitekeleza Ajenda ya Nishati Safi ya Kupikia
- Ofisi ya Waziri Mkuu yaipongeza Wizara kutekeleza miongozo ya ufuatiliaji na Tathmini kwa asilimia 100



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amewapongeza Watendaji wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa kuendelea kuimarisha utendaji kazi na hivyo kuifanya Sekta ya Nishati kuwa na matokeo chanya katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Dkt. Biteko ametoa pongezi hizo kufuatia tathmini ya utendaji kazi iliyofanywa na Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini katika Wizara ya Nishati ambayo imeonesha kuwa katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2024/2025 utendaji kazi wa Wizara/Taasisi umeimarika kwa zaidi ya asilimia 95.

Katika kikao cha Nne cha tathmini ya utendaji kazi wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake kilichofanyika jijini Dodoma, Dkt. Biteko amesema kuwa, tathmini hiyo inasaidia kujiimarisha hasa ikizingatiwa kuwa Sekta ya Nishati ina muhimu mkubwa kiuchumi na kijamii.

"Sekta hii ni muhimu sana nchini kwa kuwa ni Sekta ya huduma na sekta ya uchumi hivyo ikilegalega italeta malalamiko, ningependa kuona sekta hii inaendelea kuwa na matokeo mazuri kwa wananchi." Amesema Dkt. Biteko

Katika kikao hicho, Dkt. Biteko ameliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuendelea na kasi ya ukarabati wa miundombinu ya umeme pamoja na kuendelea kutafuta vyanzo vipya vya umeme.

Aidha, ameupongeza Wakala wa Nishati Vijijini (REA), kwa kasi iliyofanya ya kupeleka umeme vijijini na kuwezesha vijiji vyote kupata umeme pia kwa kuendelea na kasi ya kupeleka umeme vitongojini.

Kuhusu Nishati Safi ya Kupikia, Dkt. Biteko amezitaka Taasisi zilizo chini ya Wizara hususan, REA, TPDC na TANESCO kuunganisha nguvu katika kutekeleza Ajenda ya Nishati Safi ya Kupikia ili ikue na kufanikiwa na hivyo kutimiza lengo la Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan la kuhakikisha kuwa wananchi wanahama kutoka matumizi ya Nishati isiyo safi kwenda kwenye matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia.



Dkt. Biteko amekipongeza Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini katika Wizara ya Nishati kwa kutekeleza jukumu lao kwa ufanisi na kukumbusha Watendaji wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake kuwa, zoezi hilo la tathmini linapaswa kuwa ni endelevu kutokana na umuhimu wake katika kuboresha utendaji kazi.

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith.Kapinga kwa upande wake, amezipongeza Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Nishati pamoja na Idara na Vitengo vya Wizara ya Nishati kwa utendaji kazi wenye kuleta matokeo kama ambavyo tathmini ya utendaji kazi iliyotolewa ilivyoonesha kuwa ufanisi wa kazi umeendelea kuimarika.

Aidha amezitaka Taasisi chini ya Wizara ya Nishati kuibeba Ajenda ya Nishati Safi ya Kupikia ili kufikia lengo la Serikali la kufikisha asilimia 80 ya Watanzania wanaotumia Nishati Safi ya Kupikia ifikapo 2034.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba alisema kuwa kikao hicho cha tathmini ya utendaji kazi wa Wizara na Taasisi zake ni cha nne kutoka vikao vivyo vimeanza kufanyika.

Alieleza kuwa, kutoka zoezi la kupima utendaji kazi wa Wizara na Taasisi lianze kufanyika limeleta ufanisi hasa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali pamoja na mipango ya Wizara.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji wa Serikali, kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Bi. Sakina Mwinyimkuu ameipongeza Wizara ya Nishati kwa kutekeleza miongozo iliyowekwa na Ofisi hiyo ya ufuatiliaji na tathmini ambapo ameeleza kuwa Wizara ya Nishati imetekeleza miongozo iliyowekwa kwa asilimia 100.

Pia amempongeza Dkt. Doto Biteko kwa dhamira yake ya dhati katika kusimamia utendaji kazi wa Serikali hasa Sekta ya Nishati



ambayo anaisimamia akiwa ni Waziri wa Nishati.

Vilevile, ameipongeza Wizara ya Nishati kwa kutoa motisha kwa Taasisi na Idara/Vitengo zilizofanya vizuri zaidi katika tathmini ya utendaji kazi hali ambayo inaongeza ari ya kazi.

Taasisi zilizofanya vizuri Katika tathmini ya utendaji kazi iliyofanyika katika robo ya tatu ya mwaka 2024/2025 ni Wakala wa Nishati Vijijini (REA) aliyeshika nafasi ya kwanza, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) aliyeshika nafasi ya pili na Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) aliyeshika nafasi ya tatu.

Aidha, Idara/Vitengo vya Wizara ya Nishati vilivyofanya vizuri Katika tathmini ya utendaji kazi iliyofanyika katika robo ya tatu ya mwaka 2024/2025 ni Kitengo cha Ugavi na Manunuzi (nafasi ya kwanza), Kitengo cha Sheria (nafasi ya pili), na Kitengo cha TEHAMA (nafasi ya tatu).

Mikoa ya Kitanesco iliyofanya vizuri katika tathmni ya utendaji kazi ni Manyara (nafasi ya kwanza), Arusha (nafasi ya pili) na Simiyu (nafasi ya tatu).

Hata hivyo ilielezwa kuwa kwa ujumla ufanisi wa utendaji kazi wa Idara na Vitengo vya Wizara pamoja na Taasisi zake umeendelea kuimarika kwa zaidi ya asilimia 95.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt, James Mataragio, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, Menejimenti ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake pamoja na Mameneja wa Mikoa wa TANESCO.









# DKT BITEKO MGENI RASMI NISHATI BONANZA 2025

- Nia ni kuhakikisha Bara la Afrika linatumia nishati kwa ufanisi na kupunguza upotevu wa umeme
- Ni la pili kufanyika tangu kuasisiwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe Dkt Doto Biteko anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika Bonanza la Wizara ya Nishati na Taasisi zake litakalofanyika jumamosi Juni 28, 2025 jijini Dodoma.

Akizungumzia maandalizi ya Bonanza hilo, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Wizara ya Nishati, Bi. Neema Mbuja amesema kuwa, Nishati Bonanza litafanyika kwenye Viwanja vya Jamhuri mjini Dodoma na kushirikisha taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati na wadau kutoka Wizara nyingine.

" Nipende kuchukua fursa hii kuzikaribisha taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati kushiriki kikamilifu bonanza ambalo linaleta fursa ya kufahamiana na kubadilishana mawazo baada ya muda wa kazi pamoja na kufanya mazoezi ili kujenga afya." Amesema Mbuja

Ameongeza kuwa, kwa mwaka huu Nishati Bonanza linaongozwa na kauli mbiu ya "Michezo kwa Afya bora, Shiriki uchaguzi 2025 ikiwa na lengo pia la kuhamasisha wafanyakazi na wananchi kwa ujumla kutumia haki yao ya kikatiba kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 .

Amesema maandalizi yote yameshakamilika na timu zitakazoshiriki michezo mbalimbali zimeshawasili Dodoma kushiriki bonanza hilo litakaloshirikisha watu takribani 1000.

Ametaja michezo itakayoshindaniwa kuwa ni ni pamoja na Mpira wa miguu, Mpira wa Pete, Mpira wa Wavu, Mpira wa Kikapu, Kuvuta Kamba, pamoja na michezo ya jadi kama vile bao na drafti, pia kufukuza kuku.

Taasisi zitakazoshiriki Bonanza hilo la Nishati ni pamoja na TANESCO, REA, TPDC, PURA, EWURA, TGDC, ETDCO, TCPM, TANOIL, GASCO, PBPA.

Hili ni Bonanza la pili kufanyika tangu kuasisiwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe.



# WIZARA YA NISHATI TEMBEENI KIFUA MBELE MNAFANYA KAZI NZURI - DKT BITEKO

- Asema Nishati ni Sekta inayokua  kwa kasi; anajivunia kufanya nayo kazi
- Asema Rais Samia amekuwa mstari wa mbele kuiwezesha Sekta kusonga mbele
- Afunga rasmi Nishati Bonanza 2025
- TANESCO, TPDC zang'ara michezo ya Wavu Kikapu na Kamba
- Wakuu wa Taasisi waipongeza Wizara ya Nishati kuandaa Bonanza lililofana
- Mbio za wenye umri mkubwa zawa kivutio Nishati Bonanza



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema Sekta ya Nishati ni miongoni mwa sekta zinazotajwa kukua kwa kasi ya asilimia 14.7 ukiacha ile ya Sanaa na Burudani inayokua kwa asilimia 17 na hivyo kuwa miongoni mwa sekta zinazofanya vizuri hapa nchini.

Dkt Biteko ameyasema hayo Juni 28, 2025 wakati akifunga Bonanza la Nishati kwa mwaka 2025 ambalo ameliasisi likishirikisha Wizara ya Nishati na taasidi zilizo chini ya Wizara ya Nishati.

" Ndugu zangu nipende kuwapongeza sana Wizara na taasisi zake kwa kazi nzuri na kubwa mnayoifanya kuwahudumia Watanzania na mimi kama kiongozi wenu najivunia sana kufanya kazi na Wizara hii na kama kuna mahali najivunia ni ufanyaji kazi wenu kama Wizara chini ya Katibu Mkuu Mha . Felchesmi Mramba."' Amesema Mhe. Biteko

Amesema, Rais, Dkt Samia Suluhu Hassan amekuwa mstari wa mbele kuiwezesha sekta ya nishati kufanya vizuri kwa kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ambapo amewaasa Watendaji kutembea kifua mbele kwani kazi wanayofanya ni njema na imeleta matokeo chanya kwa wananchi hususani kusambaza umeme vijijini na kuongeza kuwa, Tanzania imekuwa mfano kwa nchi nyingine Afrika kutekeleza mpango wa misheni 300 wa kupeleka umeme Waafrika milioni 300 ifikapo 2030.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha Felchesmi Mramba alisema Bonanza la mwaka huu limekuwa na ongezeko la idadi ya washiriki kutokana na mwamko wa taasisi chini ya Wizara ya Nishati kuleta watu wengi zaidi ikilinganishwa na mwaka jana ambapo mwaka huu idadi ya washiriki imefikia watu 1000.

Amesema Bonanza hilo lilikuwa na kaulimbiu, Michezo kwa Afya Bora, Shiriki Uchaguzi 2025.





Katika bonanza hilo michezo mbalimbali ilishindaniwa ikiwemo mpira wa miguu, pete, wavu, kikapu, kuvuta kamba, kupenya kwenye pipa, kukimbia na yai mdomoni, karata, bao, drafti.

Mshindi wa mpira wa kikapu kwa Wanaume na wanawake alikuwa ni TANESCO, na kwa upande wa mpira wa wavu wanawake na wanaume TANESCO pia imeibuka kidedea.

Kwa upande wa mpira wa Miguu mshindi wa kwanza ni TANESCO na wa pili ni TPDC. Kwa upande wa mpira wa kamba wanaume mshindi wa kwanza ni TPDC akifuatiwa na TANESCO, kwa upande wa wanawake kamba mshindi wa kwanza ni TPDC na wa pili ni EWURA.

Katika hatua nyingine, Wizara ya



Nishati kupitia Katibu Mkuu, Mha. Felchesmi Mramba amemkabidhi Naibu waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt Doto Biteko Tuzo maalumu kwa kutambua mchango wake kwenye sekta ya Nishati na kwa kuwa muasisi wa Nishati Bonanza.

# MATUKIO KATIKA PICHA - BONANZA LA NISHATI DODOMA


















# MATUKIO KATIKA PICHA - BONANZA LA NISHATI DODOMA






























# ZAIDI YA SHILINGI BILIONI 107 ZAKAMILISHA USAMBAZAJI UMEME VIJIJINI SIMIYU

- Kapinga asema sasa Serikali inapeleka umeme kwenye Vitongoji 638
- Ataja miradi ya kuimarisha umeme Simiyu
- Simiyu yapata mitungi ya gesi 16,275 kwa bei ya ruzuku



Naibu Waziri Nishati, Mhe. Judith Kapinga amesema Serikali kupitia Wizara ya Nishati imetumia takribani shilingi bilioni 107.36 kupeleka umeme kwenye Vijiji vyote 474 vya Mkoa wa Simiyu.

Kapinga ameyasema hayo leo Juni 18, 2025 wakati akitoa tathmini ya hali ya upatikanaji wa umeme Mkoa wa Simiyu na maendeleo ya usambazaji wa nishati safi ya kupikia wakati wa kuhitimisha ziara ya kikazi ya Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Mkoa wa Simiyu.

"Mheshimiwa Rais baada ya kumaliza upelekaji wa umeme kwenye Vijiji, hivi sasa tunapeleka umeme kwenye Vitongoji na hivi sasa tunatekeleza miradi ya umeme kwenye Vitongoji 638 kati ya Vitongoji 1,408 vya Mkoa wa Simiyu". Amesema Mhe. Kapinga

Ameongeza kuwa Serikali itajenga kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Simiyu kupitia mradi wa gridi imara na kuongeza kuwa hivi sasa Mkoa wa Simiyu unapata huduma ya umeme kutoka Mikoa mitatu ya Shinyanga, Mwanza na Mara.

Amesema kituo hicho kitazidi kuimarisha hali ya umeme Simiyu na hivyo kuwa muhimu kwa maendeleo ya watu wa Simiyu.

Amesema mradi wa gridi imara mkoani Simiyu una sehemu mbili ambazo ni ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Ibadakuli Shinyanga hadi Bariadi utakaojengwa kwa takribani shilingi bilioni 48 na ujenzi wa kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Bariadi kitakachojengwa kwa gharama ya shilingi bilioni 49.

Ameongeza kuwa, kukamilika kwa mradi wa kituo cha kupokea na kupoza umeme Mkoa wa Simiyu utawezesha Mkoa kuwa na uwezo wa megawati 150.

Kuhusu Nishati Safi ya Kupikia, Kapinga amesema Mkoa wa Simiyu umepata mitungi ya gesi ya ruzuku takribani 16,275 ambayo yote tayari imeshachukuliwa na wananchi kwa bei ya ruzuku.



# BEI YA KUJAZA GESI (LPG) KWA MATUMIZI YA KUPIKIA NI HIMILIVU – KAPINGA

- Wizara ya Nishati na TAMISEMI zaendelea kushirikiana kuhakikisha Shule mpya zinafungwa mifumo ya Nishati Safi ya Kupikia

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga amesema gharama ya kujaza gesi kwenye mitungi (LPG) ni himilivu ikiwa ni jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ili kuwezesha matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia.

Mhe. Kapinga ameyasema hayo leo Juni 16, 2025 katika ziara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan mkoani Simiyu wakati wa kuzindua Shule Maalum ya Sayansi ya Wasichana ya Simiyu ambayo imefungwa miundombinu ya nishati safi ya kupikia.

"Mheshimiwa Rais ulituelekeza Taasisi ambazo zinahudumia watu zaidi ya mia moja tuzifungie miundombinu ya nishati safi ya kupikia, Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na TAMISEMI tunatekeleza agizo hilo kwa kuzifungia mifumo ya nishati safi shule mpya ambazo zinajengwa." Amesema Kapinga

Ameeleza kuwa, uwezo wa shule hiyo ni wanafunzi 800 na mifumo ya Nishati Safi ya Kupikia iliyofungwa ina uwezo wa kuhudumia wanafunzi 800.

Ameongeza kuwa, kwa idadi hiyo ya wanafunzi 800 mtungi wa gesi katika Shule ya Wasichana Simiyu utakuwa ukijazwa kila baada ya miezi miwili.






# VITONGOJI 284 ARUMERU MASHARIKI VYAFIKIWA NA UMEME

- Ni kati ya Vitongoji 330 vya Jimbo la Arumeru Mashariki.
- Kapinga asema upelekaji umeme unafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha



Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga amesema Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) imevifikishia huduma ya umeme Vitongoji 284 katika Jimbo la Arumeru Mashariki kati ya Vitongoji 330.

Mhe. Kapinga ameyasema hayo leo Juni 03, 2025 bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la Mbunge wa Arumeru Mashariki, Mhe. Dkt. John Danielson Pallangyo aliyeuliza ni lini Serikali itakamilisha kusambaza umeme wa REA katika Vitongoji 37 ambavyo vipo gizani katika Jimbo la Arumeru Mashariki.

"Mheshimiwa Mwenyekiti, Vitongoji 17 vipo katika hatua ya utekelezaji kupitia Mradi wa Ujazilizi (Densification IIB) na mradi wa kupeleka umeme katika Vitongoji Awamu ya Pili A (HEP IIA), aidha, katika Vitongoji 29 zabuni imetangazwa ili kupata Wakandarasi wa kutekeleza miradi kupitia mradi wa kupeleka umeme Vitongojini Awamu ya Pili B (HEP IIB).

Amesema kukamilika kwa miradi hiyo, kutawezesha vitongoji vyote vya Jimbo la Arumeru Mashariki kufikiwa na umeme.

Akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Arumeru Mashariki, Mhe. Dkt.John Danielson Pallangyo aliyeuliza kuhusu Kata za Arumeru Mashariki zinazo pata maji kutoka msitu wa mlima Arumeru na kuwa na flouride ambapo Kampuni ya Kweka imejitolea kuweka mtambo wa kusafisha lakini kinachohitajika ni umeme, Mhe. Kapinga amesema tayari Serikali imetenga fedha katika mwaka ujao wa fedha kukipelekea umeme wa uhakika Kitongoji cha Seneto Kata ya Legeruki kwa ajili ya kutibu flouride katika maji.

Akijibu swali la Mbunge wa Moshi Vijijini, Mhe. Profesa Patrick Alois Ndakidemi aliyeuliza Serikali itakiunganishia lini umeme Kitongoji cha Orera kilichopo Kijiji cha Mweka, Mhe. Kapinga amesema katika Jimbo la Moshi Vijijini yupo Mkandarasi anayetekeleza miradi ya kupeleka umeme kwenye Vitongoji 15 vya kila Mbunge na kuongeza kuwa kitongoji hicho kipo katika orodha hiyo ya Mkandarasi.

Akijibu swali la Mbunge wa Kondoa Mjini, Mhe. Ally Makoa aliyeuliza Serikali itapeleka lini umeme kwenye mitaa ya Mongoroma, Chandimo na Hachi, Mhe. Kapinga amesema Serikali imeipelekea umeme mitaa ya Kondoa Mjini ambapo imebaki mitaa hiyo mitatu na kuongeza kuwa itatengwa fedha katika bajeti ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuifikishia mitaa hiyo umeme.

Mhe. Kapinga ameongeza kuwa upelekaji wa umeme unafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha na bajeti ambayo imetengwa.

Akijibu swali la Mbunge wa Mwibara, Mhe. Charles Kajage aliyeuliza kuhusu lini Serikali itavipelekea umeme Vitongoji vya Jimbo la Mwibara ambavyo havina umeme, Mhe. Kapinga amesema Jimbo la Mwibara lina miradi ya Vitongoji ambayo inaendelea kutekelezwa.

Akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu, Mhe. Rita Kabati aliyeuliza kauli ya Serikali kuhusu uwepo wa nguzo Kata ya Ilula Wilaya ya Kilolo toka mwezi wa 11 mwaka jana na hadi leo umeme haujawaka, Mhe. Kapinga amesema hadi kufikia mwezi wa saba eneo hilo litakuwa limefikiwa na huduma ya umeme.

# WIZARA YA NISHATI ENDELEENI KUWEZESHA UWEKEZAJI WA VITUO VYA MAFUTA VIJIJINI- SIMBACHAWENE

- Atembelea Banda la Wizara ya Nishati na Taasisi zake katika Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene ameiasa Wizara ya Nishati kuendelea kuweka mazingira wezeshi yatakayowezesha uwekezaji zaidi wa vituo vya mafuta vijijini.

Simbachaene amesema hayo tarehe 17 Juni, 2025, jijini Dodoma wakati alipotembelea Banda la Wizara ya Nishati katika Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayoendelea katika viwanja vya Chinangali ambayo leo yamefunguliwa rasmi

" Wafanyabiashara wengi wanataka kuwekeza kwenye vituo vya Mafuta vijijini kwakuwa bado kuna uhaba wa vituo, hivyo angalieni masharti yanayowekwa kwenye uwekezaji yasiwe kikwazo kwenye huduma hii muhimu." Amesema Simbachawene

Pia, Simbachawene ameishauri Wizara kuongeza kasi ya upatikanaji wa Nishati Safi ya Kupikia Vijijini pamoja na kuhamasisha uwekezaji kwenye Nishati Safi ya Kupikia.

Vilevile, ameipongeza Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuendelea kutoa huduma za Nishati kwa wananchi.



# SEKTA YA NISHATI YACHANGIA ASILIMIA 14.4 YA PATO LA TAIFA

- Kapinga ampongeza Rais, Dkt. Samia kwa uwekezaji mkubwa katika Sekta ya Nishati
- Aeleza mafanikio yaliyofikiwa katika Umeme, Gesi Asilia na Mafuta
- Asisitiza kuwa Nishati ni moyo wa uchumi

Naibu Waziri Nishati, Mhe. Judith Kapinga amesema Sekta ya Nishati ni moja kati ya Sekta tatu nchini ambazo zimechangia ukuaji wa pato la Taifa katika kipindi cha kati ya mwaka 2015 hadi 2025.

Kapinga ameyasema hayo wakati akichangia hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mipango na Uwekezaji Bungeni Jijini Dodoma.

"Mheshimiwa Mwenyekiti ukiangalia kwa tathmini kati ya mwaka 2024 hadi 2025 Sekta ya Nishati imefanya vizuri katika kuchangia pato la Taifa, Sekta hii imetoka asilimia 5.8 mwaka 2015 na sasa hivi tunazungumzia asilimia 14.4". Amesema Mhe. Kapinga

Ameongeza kuwa, Sekta ya Nishati imeweza kufanikiwa kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanyika katika miradi ambapo amepongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji huo mkubwa.

"Katika Gesi na Mafuta yamepatikana mafanikio makubwa sana ikiwemo uendelezaji wa miradi ya uzalishaji na usafirishaji wa gesi asilia, katika kitalu cha Mnazibay na Songosongo Serikali imeweza kuzalisha futi za ujazo bilioni 25.51 kwa kipindi cha miaka minne kwa kila kimoja.

Ameongeza kuwa, Serikali



imesaini mkataba katika kitalu cha Ruvuma Ntorya na sasa hivi kipo katika hatua za awali katika kuzalisha na kuendeleza gesi asilia.

Amesema katika kipindi cha miaka minne Sekta ya Nishati imepata mafanikio makubwa kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) ambapo Serikali imeweza kuongeza hisa katika kitalu cha MnaziBay kutoka asilimia 20 hadi kufikia asilimia 40.

Ameeleza kuwa, Sekta ya gesi asilia ni muhimu kutokana na kuchagiza matumizi ya sekta nyingine ikiwemo matumizi ya gesi iliyoshindiliwa katika magari na kuunganisha mtandao wa gesi majumbani, miradi ambayo inafanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara na Lindi.

Akielezea kuhusu mafuta amesema Serikali imekuwa na mafanikio katika kusimamia na kudhibiti bei kikomo za bidhaa za mafuta na kuongeza kuwa bei ya ndani ya bidhaa za mafuta imeendelea kuwa himilivu kutokana na Serikali kuweka ruzuku kwenye bidhaa hiyo.

Kuhusu mfumo wa pamoja wa kuagiza mafuta amesema kuwa umeendelea kuimarika.

Kuhusu Sekta ya umeme, Kapinga amesema kuwa Sekta hiyo ni moyo wa uchumi katika Taifa na kutanabaisha kuwa, mwaka 2021 uwezo wa kuzalisha umeme ulikuwa takribani megawati 1,600 na hivi sasa ni takribani megawati 4,000.

Ameeleza kuwa, kuongezeka kwa megawati hizo kunatokana na uwekezaji mkubwa ambao Serikali imeufanya katika miradi ya kuzalisha umeme ukiwemo mradi wa kimkakati wa Julius Nyerere.

Kwa upande wa miradi ya usafirishaji umeme, Kapinga amesema njia za kusafirisha umeme zilikuwa kilometa takribani 6,000 mwaka 2021 na sasa hivi zipo kilometa takribani 8,000 na njia za usambazaji zimetoka kilometa 144,000 hadi kilometa 200,000.

Akielezea miradi ya umeme Vijijini, Kapinga amesema kwa kipindi cha miaka minne Serikali imekamilisha upelekaji wa umeme katika Vijiji vyote na hivi sasa Serikali imejikita kupeleka umeme katika Vitongoji.



# TANZANIA NA BENKI YA DUNIA WAJADILIANA UTEKELEZAJI MPANGO MAHSUSI WA NISHATI WA MISHENI 300

- Ufanisi wake watambuliwa Jukwaa la Nishati Afrika
- Lesotho kujifunza Tanzania utekelezaji miradi ya Nishati
- Yaahidi kuendelea kuiunga mkono Tanzania

Ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya Sekta ya Nishati nchini ikiwemo ukamilishaji wa mradi wa usambazaji umeme katika Vijiji 12,318 umekuwa kivutio katika Jukwaa la Nishati Afrika linalofanyika nchini Afrika Kusini.

Kutokana na ufanisi huo unaojumuisha ukamilishaji wa mradi wa umeme wa Julius Nyerere wa megawati 2, 115 na baadhi ya miradi ya kikanda ya usafirishaji umeme, imepelekea nchi ya Lesotho kueleza nia yake ya kuja Tanzania ili kujifunza masuala mbalimbali yatakayoboresha hali ya umeme nchini humo.

Akizungumza katika Mkutano wa Jukwaa la Nishati Afrika jijini Cape Town nchini Afrika Kusini, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba ameeleza kuwa Watanzania wanapaswa kujivunia jinsi Sekta ya Nishati inavyofanya vizuri na kuwa nchi ya mfano barani Afrika.

"Watanzania wanaweza wasifahamu sana suala hili lakini Tanzania inatazamwa sana na mataifa mengine hasa katika eneo la nishati ambalo tunaendelea kufanya vizuri." Amesema Mhandisi Mramba



Amesema kutokana na sekta ya nishati nchini kufanya vizuri, Wawakilishi wa Serikali kutoka nchini Lesotho katika Jukwaa hilo la Nishati Afrika wameeleza nia ya kuhitaji Tanzania kusaidiana nao katika maeneo yatakayoboresha hali ya umeme nchini humo.

Mramba ameeleza kuwa sekta ya nishati ni sekta muhimu inayoshikilia uchumi wa nchi kwani kukua kwa uchumi kunategemea uwepo wa nishati ya kutosha na ya uhakika.

Katika Jukwa hilo la Nishati Afrika, Mramba ameeleza umuhimu wa kushirikisha sekta binafsi kwenye miradi ya Nishati.

Ametanabaisha kuwa, kutokana na hali ya ukuaji wa uchumi nchini, Tanzania kwa upande wake inaendelea kuongeza nguvu katika maeneo ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme hivyo ushiriki wa sekta binafsi ni muhimu.

Katika ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha umeme, amewakaribisha wawekezaji kuwekeza kwenye eneo hilo akieleza kwamba Serikali pia imejipanga kuendelea kuunganisha Tanzania na nchi nyingine ambapo kwa sasa gridi ya umeme ya Tanzania imeunganishwa na gridi za Kenya, Rwanda na Burundi na hatua zinazofuata ni kuzifikia Zambia na Uganda.

Katika Jukwa hilo la Nishati Afrika, Watendaji kutoka Tanzania wamepata fursa ya kukutana na kufanya mazungumzo na wawekezaji mbalimbali waliooonesha nia ya kuweka Tanzania katika sekta ya nishati.










# TANZANIA NA BENKI YA DUNIA WAJADILIANA UTEKELEZAJI MPANGO MAHSUSI WA NISHATI WA MISHENI 300

- Mhandisi Mramba aeleza hatua zinazochukuliwa na Serikali kutekeleza Misheni 300
- Benki ya Dunia yapongeza
- Yaahidi kuendelea kuiunga mkono Tanzania



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felichesmi Mramba amekutana na Viongozi Waandamizi kutoka Benki ya Dunia ( WB) kwa lengo la kujadili hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa Mpango Mahsusi wa kuwafikishia umeme Waafrika milioni 300 ifikapo 2030 ujulikanao kama Misheni 300.

Kikao hicho kimefanyika katika Jiji la Cape Town nchini Afrika Kusini kando ya Mkutano wa Jukwaa la Nishati Afrika ambapo Tanzania inashiriki.

Mhandisi Mramba ameeleza kuwa, katika Mpango huo uliosainiwa katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika uliofanyika mwezi Januari 2025, Tanzania kwa upande wake imeuweka Mpango huo kwenye mipango yake ya Serikali ili kutimiza malengo yaliyowekwa.

Amesema kukamilika kwa Mpango huo kutaiwezesha Tanzania kuongeza upatikanaji umeme kutoka asilimia 78.4 ya sasa hadi asilimia 100 ifikapo mwaka 2030 na kuongeza matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia hadi kufikia asilimia 75 ifikapo 2030.

Kwa upande wao, Watendaji wa Benki ya Dunia, Bi.Yadviga Semikolenova, Meneja Mtendaji Ukanda wa Kusini Mashariki mwa Afrika pamoja na Dkt. Rhonda Antoine, Mtaalam Mwandamizi wa Nishati Ukanda wa Afrika wameipongeza Serikali ya Tanzania kwa hatua inazochukua ili kuhakikisha Mpango wa Misheni 300 unafanikiwa na hivyo kuwezesha wananchi kupata nishati ya uhakika.

Aidha, Benki ya Dunia imeonyesha utayari wa kuendelea kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Tanzania kuhakikisha inaendelea kuutekeleza mpango wa Misheni 300.

Katika kikao hicho, Mhandisi Mramba aliambatana na Mhandisi Innocent Luoga, Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu pamoja na wataalam kutoka Wizara ya Nishati, TANESCO, REA, TPDC na EWURA.

# USALAMA WA NISHATI NI NGUZO MUHIMU KATIKA USALAMA WA NCHI NA MAENDELEO ENDELEVU - MHANDISI MRAMBA

- Asema Nishati sio jambo la anasa bali ni hitaji la msingi kwa maisha ya kila siku.
- Tanzania inajenga mfumo wa Nishati endelevu.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba amesema kuwa usalama wa nishati ni nguzo muhimu katika uwepo wa usalama wa nchi, maendeleo endelevu, ustawi wa jamii na uhifadhi wa mazingira hivyo kuna umuhimu wa kuendelea kuwekeza katika miradi mikubwa ya kuzalisha nishati safi na ya uhakika.

Mhandisi Mramba amesema hayo Juni 6, 2025 wakati wa Mkutano wa Kitaifa wa Usalama wa Taifa (National Security Symposium 2025) uliofanyika jijini Arusha ambao umekutanisha wataalam wa sekta ya Nishati na Usalama.

"Nishati si jambo la anasa, ni hitaji la msingi kwa maisha ya kila Mtanzania na ni injini ya maendeleo ya taifa lolote, hivyo usalama wa nishati unapaswa kuangaliwa kama ajenda ya kimkakati ya ulinzi wa Taifa," amesema Mhandisi Mramba

Ameeleza kuwa, Serikali ya Tanzania inaendelea na jitihada za kuhakikisha nchi inakuwa na nishati ya kutosha ambapo kwa sasa uwezo wa kufua umeme umefikia megawati 4,414.69 huku mahitaji ya juu zaidi ya umeme yakifikia megawati 2,316.42.

Amesema kuwa, kati ya megawati hizo, megawati 4,031.71 zinatoka kwenye gridi kuu ya taifa, megawati 243.42 zinazalishwa na sekta binafsi na megawati 52 zinatoka Zambia na Uganda.

"Mahitaji ya juu zaidi ya umeme nchini yamefikia megawati 2,316.42, huku kasi ya ukuaji wa mahitaji hayo ikikadiriwa kuwa kati ya asilimia 10 hadi 15 kila mwaka hivyo tunachukua hatua madhubuti kuhakikisha tuna mchanganyiko imara wa vyanzo vya nishati ili kupunguza utegemezi kwa chanzo kimoja na kuongeza uthabiti wa mfumo wetu," Ameeleza Mhandisi Mramba

Mhandisi Mramba ameeleza kuwa Tanzania imeanza vizuri safari ya kujenga mfumo wa nishati endelevu ingawa bado kuna safari ndefu, akieleza kuwa kwa sasa wateja zaidi ya milioni 5.44 wameunganishwa na umeme, kiwango cha upatikanaji wa huduma ya umeme kimefikia asilimia 78.4 mwaka 2020 na kaya zilizounganishwa na umeme zikiwa asilimia 46.

Kuhusu umeme katika Bara la Afrika amesema kuwa zaidi ya watu milioni 600 hawajaunganishwa na huduma ya umeme hivyo unahitajika mwelekeo wa pamoja wa Bara zima kuhakikisha kila mtu anapata huduma ya nishati safi, salama na nafuu.

Katika mkutano huo, Mhandisi Mramba ametoa angalizo kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili kwa usalama wa nishati akisema kuwa "uharibifu wa mazingira na ukame unaoathiri vyanzo vya maji ni tishio halisi, tusipowekeza kwenye mchanganyiko wa nishati na teknolojia mpya, tutakuwa hatarini kiusalama na kiuchumi."

Hata hivyo amesema kuwa, kwa mwaka 2025 pekee, Dunia imewekeza Dola za Marekani trilioni 2.2 katika teknolojia safi za nishati, ikiwa ni mara mbili ya uwekezaji unaofanywa kwenye mafuta ya visukuku na hiyo ikionesha kuwa mwelekeo wa dunia sasa ni kuelekea kwenye uzalishaji wa nishati safi hivyo Tanzania haiwezi kubaki nyuma.

Mramba pia amesisitiza kuhusu ushirikiano wa kikanda kupitia miundombinu ya nishati inayounganisha nchi na nchi ili kuhakikisha kunakuwa na usalama wa nishati hata wakati wa changamoto.

Pia ametoa wito kwa sekta binafsi kuwekeza zaidi katika Sekta ya Nishati kupitia ubia na Serikali (PPP), akieleza kuwa Serikali peke yake haiwezi kukidhi mahitaji ya nchi hivyo inahitaji uwekezaji kutoka kwa kila mdau mwenye dhamira njema ya kujenga taifa lenye nishati ya uhakika.

# MFUMO WA MPYA WA UWEKEZAJI WA TANESCO UTALETA MAPINDUZI YA UWEKEZAJI SEKTA YA UMEME - MHE. KAPINGA

- Asema utasaidia kuvutia wawekezaji katika Miradi ya umeme
- Asisitiza utaongeza uwazi na kupunguza urasimu kwa wawekezaji

Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga amesema mfumo mpya wa uwekezaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wa uwekezaji unaofahamika kama TIMS yaani (TANESCO INVESTMENT MANAGEMENT SYSTEM) utaleta mapinduzi makubwa katika sekta ya uwekezaji kwenye sekta ya umeme nchini.

Mhe. Kapinga amesema hayo leo Juni 25, 2025 wakati akizindua mfumo huo alipomuakilisha Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko ambapo amesema mfumo huo umelenga kuongeza ufanisi na kupunguza urasimu kwa kuwa utamuwezesha muwekezaji kupata taarifa za moja kwa moja kuhusu miradi inayofaa kwa ajili ya uwekezaji kwa haraka na kwa usahihi zaidi.

"Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea kuweka mazingira mazuri na rafiki kwa uwekezaji. Mifumo kama hii inayotumia teknolojia itasaidia kuondoa urasimu na kutoa nafasi kwa wawekezaji kuwasiliana moja kwa moja na Shirika kwa hatua za haraka zaidi,"amefafanua Mhe.Kapinga.

Akizungumza kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO Mhandisi Isaac Chanji amesema mfumo huo utaongeza imani kwa wawekezaji wenye nia ya kushiriki miradi ya kimkakati ambapo mpaka sasa jumla ya miradi minne tayari imeingizwa kwenye mfumo huo.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO Bw. Lazaro Twange amefafanua kuwa mfumo huo utasaidia kuongeza uwazi, uwajibikaji na kuongeza hofu kwa wale wenye nia ya kufanya uovu kwa sababu kila kitu kinafanyika kwa uwazi.

"Zipo nyakati ambazo ofisi za umma hazisemwi vizuri kutokana na urasimu. Sasa mfumo wa TIMS utaondoa kabisa changamoto hiyo kwakua taarifa zote za fursa za uwekezaji zitajumuishwa na hata wawekezaji wataomba kupitia mfumo huo kwa kuingiza taarifa zao," amesisitiza Bw. Twange.

Kwa upande wake Naibu Mkurugenzi Mtendaji, Mipango, Utafiti na Uwekezaji, CPA Renatha Ndege amesema kuanzishwa kwa mfumo huo pia kumeakisi mkakati wa TANESCO wa kuendana na matumizi ya teknolojia katika shughuli zake.

"Wawekezaji wanaweza kuona miradi ya uwekezaji ya nishati wanayoweza kushirikiana na TANESCO , ili waweke ze ,Ndani ya mfumo wa TIMS kutakuwa na taarifa za miradi mikubwa na kimkakati" Alisisitiza Bi. Ndege.

Mfumo huu ni miongoni mwa mikakati ya TANESCO ya kuvutia wawekezaji katika sekta ya umeme nchini pamoja na kukuza ushirikiano baina yake na sekta binafsi katika kufanikisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umeme nchini.

# DKT KAZUNGU AKUTANA NA WAWEKEZAJI KUTOKA JAPAN, WAAHIDI KUWEKEZA KWENYE MIRADI YA UMEME

- Pia kuwekeza kwenye miundombinu ya usafirishaji umeme nchini
- Waialika Tanzania kushiriki mkutano wa Tisa wa maendeleo kati ya Japan na Afrika
- Waupongeza mpango mahsusi wa Nishati wa Taifa kuwa bora na wa mfano kwa nchi za Afrika



Naibu katibu Mkuu Wizara ya Nishati, anayeshughulikia umeme na nishati jadidifu Dkt Khatibu Kazungu, leo amekutana na kuzungumza na ujumbe wa wawekezaji kutoka nchini Japan kupitia kampuni ya Toyota Tshusho Cooperation, uliolenga kufanya mazungumzo kuhusu uwekezaji wa miradi mbalimbali kwenye sekta ya umeme hususan umeme wa jua, upepo na njia za kusafirisha umeme pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme chini ya mpango mahsusi wa Nishati wa Taifa ujulikanao kama Energy Compact.

Kupitia serikali ya Japan chini ya Japan International Banking Corporation, Japan imeonesha nia yake ya kuwekeza kwenye maeneo hayo na kwa sasa wapo kwenye mazungumzo na Serikali ya Tanzania ili kuainisha maeneo hayo ya uwekezaji.

Dkt Kazungu amesema Japan imeonesha nia hiyo ya kuwekeza chini ya mpango huo mahsusi kutokana na Tanzania kuwa na mpango mzuri wa ajenda ya Compact ambao umekuwa wa mfano kwa nchi za Afrika hususan kwenye mafanikio kuunganisha umeme kwa wateja, na nchi nyingi za Afrika zimekuwa zikijifunza kutoka mpango wa Tanzania.

Mpango mahusus wa Nishati wa Taifa ulibuniwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Benki ya Dunia kwa lengo la kuzisaidia nchi za Afrika kutekeleza miradi mbalimbali ya nishati wakati wa mkutano wa wakuu wa nchi uliofanyika jijini Dar es salaam wa Mission 300 uliobeba ajenda ya kuhakikisha waafrika milioni 300 wanafikiwa na umeme ifikapo mwaka 2030.

Katika hatua nyingine Serikali ya Japan imeialika Tanzania kushiriki kwenye mkutano wa tisa wa masuala ya maendeleo kwa nchi za Afrika utakaofanyika nchini Japan mwezi Agosti, 2025 kwa lengo la kuzikutanisha nchi za Afrika kujadili masuala ya maendeleo kwenye sekta mbalimbali.





# KAMPENI YA PIKA SMART INAYOHAMASISHA MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA YAZINDULIWA

- Kamishna Luoga asisitiza matumizi ya umeme katika Nishati Safi ya Kupikia

Kamishina wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga amezindua kampeni ya kitaifa ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ya umeme inayokwenda na kaulimbiu ya PIKA SMART.



Mha. Luoga amezindua kampeni hiyo leo Juni 13, 2025 jijini Dar es Salaam akimwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba.

Kampeni hiyo imeandaliwa na Shirika la Modern Energy Cooking Services (MECS) chini ya ufadhili wa UKAID kwa kushirikiana na Serikali kupitia Wizara ya Nishati.

Mhandisi Luoga amesema kampeni hiyo imezinduliwa ikiwa ni mojawapo ya jitihada za Serikali kuhakikisha inawahamasisha wananchi kutumia nishati safi ya kupikia ili kufikia lengo la asilimia 80 ya watanzania kutumia nishati safi ya kupikia ifikapo 2034.



Luoga amewatoa hofu wananchi kuhusu kutumia nishati safi ya kupikia ya umeme akitanabaisha kuwa ni salama na gharama nafuu na kuongeza kuwa Tanzania Ina Umeme mwingi na wa kutosheleza mahitaji.

“Kama tunavyofahamu bwawa la kufua umeme kwa maji la Julius Nyerere limekamilika na hivyo kupelekea umeme uliopo nchini hadi sasa kufikia takribani megawati 4,031, umeme huu umeshafika katika Vijiji vyote






12, 318 vya Tanzania hivyo kuna kila sababu kwa wananchi kutumia nishati safi ya umeme kupikia." amesema Mha. Luoga
.
Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji TANESCO, Mkurugenzi wa Mipango na uwekezaji TANESCO, Mhandisi Henryfried Byabato amesema Shirika hilo limekuwa likihamasisha wananchi kutumia nishati safi ya kupikia ya umeme kutokana na uwepo wa kutosha wa nishati hiyo nchini.

Ameongeza kuwa, teknolojia zimeboreshwa hivyo majiko ya umeme yanatumia nishati kidogo na kwa ufanisi mkubwa.

Kampeni hii ya kuhamasisha matumizi ya pika smart imekuja wakati muafaka ambapo Wizara ya Nishati imezindua mkakati wa Taifa wa Mawasiliano wenye lengo la kutoa mwongozo kwa wadau kuendeleza kampeni ya uhamasishaji matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan ambaye ni kinara wa nishati safi ya kupikia kuhakikisha watanzania wanahama kutoka kwenye matumizi ya nishati isiyo safi kwenda kwenye nishati safi.

# WIZARA YA NISHATI KATIKA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA DODOMA

Marukio mbalimbali wakati Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu Wizara ya Nishati, Ziana Mlawa alipotembelea Banda la Wizara ya Nishati na Taasisi zake katika Maadhimisho ya Kitaifa ya Wiki ya Utumishi wa Umma 2025 yanayoendelea katika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma.








# WIZARA YA NISHATI NA TAASISI ZAKE YASHIRIKI MAADHIMISHO YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA DODOMA

Wizara ya Nishati na taasisi zilizo chini yake inashiriki Maadhimisho ya Kitaifa ya Wiki ya Utumishi wa Umma ambayo yameanza Juni 16, 2025 katika viwanja vya Chinangali, Jijini Dodoma.

Maadhimisho hayo yamebebwa na kaulimbiu isemayo “Himiza Matumizi ya Mifumo ya Kidijiti Kuongeza Upatikanaji wa Taarifa na Kuchagiza Uwajibikaji”,

Watalaam wa Wizara pamoja na kueleza mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Nishati ikiwemo ukamilishaji wa mradi wa umeme wa Julius Nyerere na usambazaji wa umeme vijijini, wanatoa elimu kwa njia mbalimbali ikiwemo machapisho na vitendo kuhusu ajenda ya kitaifa ya utekelezaji wa Mkakati wa Nishati Safi ya kupikia.

Taasisi za Wizara ya Nishati zinazoshiriki maadhimisho hayo ni Shirika la Umeme Tanzania ( TANESCO), Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli ( PURA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania ( TPDC), Wakala wa Nishati Vijijini ( REA) na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA).











